ictj briefing

“Kuishi Kama Wakenya Wengine”: Utafiti Kuhusu Madai ya Waathiriwa wa Ukiukaji Haki za Binadamu Nchini Kenya

ICTJ Kenya
kenyainfo@ictj.org

Aug 2011

YALIOMO

Kuhusu Utafiti juu ya Ufidiaji 1
Kuhusu Waathiriwa Walioshiriki katika Utafiti Huu 2
Matokeo ya Utafiti 2
Mapendekezo 3
Shukrani 4

Kuhusu Utafiti juu ya Ufidiaji (About the Study)

Ufidiaji ndiyo njia ya haki ya kipindi-mpito inayolenga zaidi waathiriwa. Nchini Kenya, kuzingatiwa hapo awali kwa haki ya kipindi-mpito kumetilia maanani zaidi Tume ya Ukweli, Haki na Maridhiano (Truth Justice and Reconciliation Commission - TJRC). Waathiriwa walitazama TJRC kama fursa muhimu zaidi ya kuhadithia tajriba zao kuhusiana na kukiukwa haki za binadamu. Hata hivyo, TJRC imekumbwa na tatizo la kutoaminika kutokana na sifa zisizo nzuri za kiongozi wake kuhusiana na ukiukaji wa haki za binadamu. Jambo hili limeathiri pakubwa na kwa namna mbaya taratibu za Tume. Jambo hilo limewapa wasiwasi waathiriwa kwamba Tume haina uwezo wa kutekeleza mahitaji na matakwa yao ya ufidiaji Tangu hapo, uchunguzi na harakati ambazo zimeanzishwa na Mahakama ya Kimataifa ya Jinai (International Criminal Court - ICC) kuhusiana na jinai dhidi ya binadamu ambazo labda zilifanyika wakati wa fujo za baada ya uchaguzi wa 2007 zimetiliwa maanani zaidi. Mbali na hatua hizo zinazoendelea, hakujakuwa na majadiliano mengi kuhusu ufidiaji kwa waathiriwa wa kukiukwa haki za binadamu kulikotokea wakati wa visa mbalimbali vya mikinzano na unyanyasaji humu nchini. Utafiti huu ni juhudi za kuhakikisha kwamba ufidi-

aji kwa waathiriwa ni jambo linalokubalika kama mojawapo ya malengo ya kuzingatia haki ya kipindi-mpito nchini Kenya na kwamba matokeo ya mbinu za hivi sasa na za baadaye za haki ya kipindi-mpito zinatilia maanani maoni ya waathiriwa. Taarifa hii ni muhtasari wa kile ambacho waathiriwa wamekielezea kama hatua ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kuondolea mbali athari na vilevile kushughulikia sababu za ukiukaji haki za binadamu uliowakumba waathiriwa hao.

Utafiti huu ulinuiwa kuwapa waathiriwa fursa ya kutoa maoni yao kuhusiana na njia zinazoibuka za kutekeleza haki ya kipindi-mpito. Waathiriwa waliambiwa waeleze kwa matamshi yao wenyewe mahitaji yanayotokana na maonevu waliyofanyiwa bila maelezo yao kubanwa na msamiati au mfumo wa watu wengine. Jambo hili lilifanywa kwa kutumia njia za utafiti zinazozingatia ubora kama kigezo cha uchunguzi. Waathiriwa walikutana kwenye mahojiano ya kibinafsi na kwenye majadiliano katika makundi maalum na wakaambiwa waeleze athari za ukiukaji haki na kile walichoona kama hatua za dharura zaidi zinazopaswa kuchukuliwa ili kulipia fidia. Utafiti ulifanywa mwaka wa 2010 na kulitumiwa mkabala wa muundo wa utafiti wenye uhuru wastani. Majadiliano ya hadharani yaliandaliwa na jambo hilo liliwaruhusu waathiriwa kutia mkazo mambo ambayo wao wenyewe waliyaona kuwa ni muhimu zaidi. Mahojiano na majadiliano katika makundi maalum yaliandaliwa katika maeneo sita. Waathiriwa 376 waliokumbwa na ukiukaji haki za binadamu wa aina mbalimbali walishiriki.

Kuhusu Waathiriwa Walioshiriki katika Utafiti Huu (Profile of the victims met during the study)

Waathiriwa walioshiriki walikumbwa na ukiukaji haki za kiraia au kisiasa, au wakati mwingine, aina zote mbili na vilevile ukiukaji haki za kijamii na kiuchumi. Baadhi ya walioshiriki walikuwa watu walionusurika au wale waliokuwa na jamaa waliokumbwa na mauaji ya kimakundi na mauaji ya dola yasiyo halali, mateso yaliyofanywa dola la hivi sasa na vilevile majeshi ya usalama ya kikoloni. Waathiriwa wengine walitimuliwa makwao wakati wa mapigano ya kikabila na pia wakati wa fujo zilizohusiana na uchaguzi zilizoungwa mkono na dola. Mara nyingi, fujo hizo ziliandamana na hujuma za kimapenzi na maonevu mengine ya kijinsia. Washiriki wengi walikuwa ni watu walionusurika kutokana na fujo hizo na ambao kutokana na vitendo vilivyoungwa mkono na dola, walipokonywa makwao, ardhi na mbinu nyingine za kujipatia riziki. Wengine walikuwa waathiriwa wa maonevu ya kihistoria na kutengwa kwenye mambo muhimu kunakoendelea. Mkazo ulitiliwa kwenye fujo za baada ya uchaguzi wa 2007 – 2008 ambazo zilisababisha kuwepo kwa njia za hivi sasa za kutekeleza haki za kipindi-mpito. Waathiriwa hao walikuwa asilimia 44 ya wote walioshiriki.

Matokeo ya Utafiti (Findings of the Study)

Mielekeo miwili wazi iliibuka kutoka kwa waathiriwa kuhusiana na mitazamo yao juu ya ufidiaji. Kuna mwelekeo unaolenga nyuma unaotaka dola itambue madhara yaliyowakumba waathiriwa, kurekebishwa kwa ukiukaji haki na kurejeshwa hali ya awali ya maisha yao. Mwelekeo wa pili unalenga mbele. Washiriki walitaka kukomeshwa duru za fujo na mikinzano nchini Kenya na walielezea hamu yao ya kuwa na usalama na kupata riziki na kupewa hakikisho la kutorudiwa ukiukaji haki za binadamu.

Kupata riziki kutokana na ardhi kumekuwa kiini cha visa vingi vya ukiukaji haki za binadamu vilivyoelezewa na waathiriwa walioshiriki kwenye utafiti huu. Kutokana na mitazamo yao, ugavi wa ardhi usio wa haki umekuwa chanzo na athari za ukiukaji haki wa kiwango kikubwa na wa hatua kwa hatua dhidi yao. Kunyimwa matumizi ya ardhi mara nyingi kunatekelezwa kwa kutumia nguvu na, kwa hivyo, kuingilia hadhi ya kimwili ya waathiriwa. Kila wakati jambo hili linasababisha kupotea kwa riziki na, kwa hivyo, kukiukwa haki za

kimsingi za kiuchumi na kijamii za waathiriwa. Wakati mwingine nafasi ya kutumia ardhi inapotea kupitia ufisadi au kupitia unyakuaji ardhi 'uliohalalishwa' unaopuuza mila na haki za umiliki za jamii zinazohusika. Vyovyote iwavyo, haki za binadamu zinakiukwa na ufidiaji kwa madhara yanayotokana na fujo na utumiaji nguvu – kama kuwezesha watu kuishi maisha ya kawaida na kulipa fidia – huenda yakawa mambo yasiyotosha kurekebisha madhara yaliyosababishwa na ukiukaji haki za kijamii na za kiuchumi kama vile kupoteza riziki. Ikiwezekana, kurejeshewa mali ya hapo awali ni jambo linaloweza kusuluhisha baadhi ya madhara haya. Lakini hakikisho kutoka kwa dola kwamba, kupitia hatua za kulinda nafasi ya kutumia ardhi, hakutarudiwa ukiukaji haki, ingekuwa aina ya ufidiaji ya kudumu na wenye maana.

Waadhiriwa wa ukiukaji haki wa aina zote waliyapa umuhimu zaidi masuala ya riziki wakionyesha kwamba aina zote za ukiukaji haki zinaathiri kiuchumi walionusurika. Walioathiriwa na fujo za baada ya uchaguzi waliopoteza makwao, walitilia mkazo kulipwa fidia, kupata makazi mapya, kupata ardhi na kupata usaidizi wa kufanya biashara. Kupata nyumba na ardhi au njia nyingine za kujipatia riziki yalikuwa mahitaji ya kimsingi ili kurejesha hali ya awali ya maisha. Waliotimuliwa makwao walitilia mkazo kusaidiwa kupata makazi mapya na nyumba. Waathiriwa wa hujuma za kimapenzi waliongezea kwamba wangependa kupata usaidizi wa kimatibabu na ushauri wa kisaikolojia. Waathiriwa wa utumiaji nguvu wa dola, kama vile familia za wale waliofariki katika mauaji ya kimakundi katika eneo la Kaskazini Mashariki, walitia maanani zaidi kulipwa fidia na kushtakiwa mahakamani waliotekeleza mauaji hayo kwa vile waliyaona mambo yote mawili kuwa ni aina za kutambua maovu yaliyofanyika. Ukweli na kutambua ukiukaji haki kulichukuliwa kuwa ni hatua muhimu dhidi ya mazoea ya dola ya kukana na pia ya kuruhusu ulipaji fidia.

Waathirirwa wengi walioshiriki katika utafiti walikuwa wanafuatilia harakati za Mahakama ya Kimataifa ya Jinai nchini Kenya (ICC). Walionelea kwamba jambo hilo ni sehemu muhimu ya utaratibu wa kimahakama nchini Kenya ambao haungewezana au ambao ungekuwa na upungufu mkubwa. Asilimia 82 ya wahojiwa haikuwa na imani na utaratibu wa kimahakama nchini Kenya. Asimilia 74 walitaka ICC ishiriki katika kushtaki waliotekeleza maovu. Hamu ya kushirikisha ICC kwenye ukiukaji haki za binadamu uliowaathiri wahojiwa ilikuwa na upeo mpana zaidi ya fujo za baada ya uchaguzi. Jambo hili linaonyesha ukosefu wa imani kwenye mfumo wa kulinda haki nchini Kenya na pia linaonyesha kwamba wawasi yao haikuwa juu ya fujo za baada ya uchaguzi pekee.

Katika kuelezea njia zenye maana na zinazoweza kufaa kusuluhisha maovu waliyofanyiwa, waathiriwa walioshiriki walipendekeza hatua ambazo wakati mwingine zinaafikiana na aina za ufidiaji zinazoelezewa katika *United Nations Basic Principles and Guidelines on the Right to Remedy and Reparations* (kwa kifupi, *UN Basic Principles*) ambazo ni kulipwa fidia, kuridhika, kurejeshewa hali ya kawaida ya maisha, kurejeshewa mali iliyochokuliwa na kupata hakikisho kwamba maovu hayatarudiwa. Wakati mwingine waathiriwa walipendekeza hatua – kama vile kupata riziki na kutumia ardhi na maliasili kwa amani au kurejeshewa makazi ya jamii zao – hatua ambazo zinahitaji mabadiliko ya kimsingi zaidi ya mahusiano ya kijamii na kiuchumi miongoni na baina ya Wakenya wa matabaka na makundi tofautitofauti.

Mapendekezo (Recommendations)

Mapendekezo yaliyomo katika taarifa hii yameegemezwa kwenye malengo mawili. Lengo la kwanza ni kutekeleza mradi wa dharura wa ufidiaji ambao utashughulikia mahitaji ya walio katika hatari ya kuathirika zaidi. Lengo la pili ni dola kuunda utaratibu kamili wa mradi wa ufidiaji ambamo upeo mpana wa aina za ukiukaji haki za kiraia, kisiasa na vilevile za kiuchumi na kijamii utatambuliwa na athari na sababu za ukiukaji haki kushughulikiwa kupitia hatua za ufidiaji kiishara na kwa mali. Katika kutekeleza malengo yote mawili, mapendekezo

yanatilia mkazo umuhimu wa kuwapa waathiriwa na walionusurika uhuru na nafasi ya kutoa maoni ambayo yamefafanuliwa katika utafiti huu.

Mapendekezo haya yanazingatia maoni yaliyotolewa katika makundi maalum ya majadiliano. Mahojiano na majadiliano katika makundi maalum yalisababisha kupatikana madai ya hatua za kiishara na za ki-bidhaa ambazo waathiriwa wanahitaji kutegemea hali na kiwango cha ukiukaji haki za binadamu uliowakumba washiriki na vilevile hali yao ya hivi sasa.

Mapendekezo haya hayanuiwi kuwa makamilifu au ya kuwakilisha aina yoyote au aina zote za ufidiaji ambao ni mwafaka katika muktadha wa Kenya. Mapendekezo yamewasilishwa hapa kama msingi mmojawapo wa utetezi, uundaji sera na usaidizi ambao serikali, mashirika yasiyo ya kiserikali, waundaji sera wengine na wafadhili wanaweza kutathmini kuona kama yafaa na kuyatumia.

1. Serikali inapaswa kutekeleza mradi wa mara moja wa ufidiaji (Urgent Reparations Program – URP). Mradi kama huo unaweza kutilia mkazo waathiriwa walio katika hatari zaidi ya kupata madhara wenye mahitaji ya dharura yanayotokana na ukiukaji haki wa hivi majuzi zaidi hasa ule wa fujo za baada ya uchaguzi za mwaka 2008. Mradi wa mara moja wa ufidiaji unaweza:

    1.1 Kuwapa kipaumbele wazee, wajane, wakina mama wasio na waume, mayatima, watoto wenye mahitaji maalum, waathiriwa wa dhuluma za kimapenzi na za kijinsia, na waathiriwa wenye upungufu wa kimwili au kiakili katika utoaji huduma za kiwango wastani za kulipa fidia na kuwarejeshea hali ya hapo awali ya maisha.

    1.2 Kutoa aina ya pamoja ya ufidiaji wa dharura, ikiwa ni pamoja na huduma kwa jumuia na ardhi kwa wale ambao hawawezi kutumia njia zao za asili za kujipatia riziki.

    1.3 Kujumuisha usaidizi wa kimatibabu, ikiwa ni pamoja na upasuaji, kwa wale wenye hali za kimwili zinazoweza kuangamiza maisha au ambazo zinawazuia kufanya kazi au kwenda shule au ambazo ni matokeo ya kudhulumiwa kimapenzi.

    1.4 Kujumuisha usaidizi wa kisheria kwa waliotimuliwa makwao au kwa waathiriwa wanaohitaji vitambulisho vya kiserikali, vyeti kuhusiana na uraia, vifo au vya kupotea watu, na vyeti vingine ambavyo vinaweza kuhitajika katika kutafuta usaidizi.

2. Kunapaswa kuwepo utaratibu unaoaminika wa kutafuta ukweli kwa vile ufidiaji halisi unaweza kupatikana tu kupitia matokeo ya uchunguzi halisi katika utaratibu wa Kenya wa kisheria wa kipindi mpito. Katika kufanya hivyo, serikali inapaswa:

    2.1 Kuimarisha kushiriki kwa waathiriwa kutoka upeo mkubwa wa makabila na jumuia.

    2.2 Kupata maoni ya waathiriwa wakiwa sio tu wale waliokumbwa na utumiaji nguvu wa hivi majuzi lakini pia wale walioathiriwa na ukiukaji haki wa kihistoria, wa unyakuaji ardhi, wa kutimuliwa makwao na aina nyingine za kutengwa katika jamii.

    2.3 Kuwezesha wanawake kuwasilisha taajriba zao mahsusi za kuathirika na kunusurika sio tu kuhusiana na dhuluma za kimapenzi lakini pia athari zitokanazo na ukiukaji haki za binadamu kuhusiana na majukumu yao katika familia zao na jumuia.

2.4 Kudhihirisha maoni ya waathiriwa kuhusiana na kuunda sera ya ufidiaji.

3. Marekebisho ya Katiba kuhusiana na masuala ya ardhi yanapaswa kufungamanishwa na madai ya waathiriwa juu ya ufidiaji ikiwa ni pamoja na kurejeshewa hali ya awali ya maisha na kufidiwa kwa sababu ya kukiukwa haki za kijamii na kiuchumi za familia na jumuia ambazo zimetengwa katika jamii.

    3.1 Serikali inapaswa kuwa na mkabala kamili wa kutambua na kurekebisha historia ndefu ya kutumiwa vibaya ugavi wa ardhi na inapaswa kuhakikisha kuheshimiwa lengo la Katiba la kusuluhisha utovu wa haki wa kihistoria kuhusiana na ardhi na haki za waathiriwa katika kutilia maanani madai ya kurejeshewa mali iliyochukuliwa na ugavi wa ardhi.

    3.2 Serikali inapaswa kutilia maanani sio tu matokeo ya kuaminika ya utafiti lakini pia mapendekezo ya Tume ya Haki na Maridhiano au hatua nyingine, lakini pia inapaswa kuchukua hatua kuhusiana na Tume ya Ndungu kuhusu ugavi wa ardhi ya umma ulio kinyume cha sheria na usio sawa wakati wa kutengeneza mapendekezo kuhusiana na masuala ya ardhi.

    3.3 Tume ya Taifa ya Ardhi itakayoundwa na Katiba inapaswa kupewa wajibu wazi katika kushughulikia utovu wa haki za kihistoria kuhusiana na masuala ya ardhi na kushughulikia umiliki wa kiasili na kurekebisha hati za ardhi zilizotolewa kimakosa kutokana na ufisadi.

4. Serikali inapaswa kufikiria kuunda mradi kamili wa ufidiaji

    4.1 Mradi kama huo unaweza kutumia habari za asisi za serikali ambazo, kila moja kivyake, zimeshughulikia mahitaji na wasiwasi ya waathiriwa, ikiwa ni pamoja na Tume ya Taifa ya Haki za Binadamu (KNCHR), asisi za serikali na mashirika yasiyo ya kiserikali yanayotoa makazi na huduma kwa wakimbizi wa humu nchini na, asisi za serikali na zisizo za serikali ambazo zimekuwa zikitoa usaidizi wa bidhaa, wa kisheria na wa aina nyingine kwa waathiriwa wa vipindi mbalimbali vya fujo na watu kutimuliwa makwao. Habari hizo zinaweza kutumiwa kama msingi wa juhudi zaidi za kutathmini mahitaji ya waathiriwa.

    4.2 Asisi iliyo huru inapaswa kuwa mwangalizi wa utathmini wa mahitaji ya waathiriwa na vilevile kushauriana nao kuhusu utaratibu wa usajili ambao unatangulia muundo na utekelezaji wa ufidiaji. Wawakilishi wa makundi ya waathiriwa na ya kiraia walioteuliwa kwa namna inayoshirikisha jumuia, makundi mahsusi ya waathiriwa na nyakati mbalimbali za dhuluma, wanapaswa kirasmi kuwa sehemu za uongozi na uundaji sera wa asisi hiyo.

    4.3 Iwapo tume ya ukweli au mahakama imependekeza au kuamuru ufidiaji kwa kundi lolote mahsusi la waathiriwa, serikali itatilia maanani pendekezo au amri hiyo kwenye muundo na sera ya mradi wa ufidiaji na kuhakikisha kwamba waathiriwa na wanaonufaika kutokana na ufidiaji wanapata aina yenye maana na mwafaka ya ufidiaji wa kibidhaa na wa kiishara ambao unawezekana katika hali mahsusi.

4.4 Gharama na mali nyinginezo za mradi wa ufidiaji zinapaswa kutolewa kwa mpango na dola moja kwa moja na kila mwaka. Mali zaidi inaweza kutolewa kupitia sheria, ikiwa ni pamoja na kupunguzwa deni la kigeni, kutwaaliwa mali ya maafisa wa umma iliyopatikana kwa ufisadi na jinai nyingine za kiuchumi, na mali inayotolewa na wafadhili.

4.5 Kuhusiana na wakimbizi wa humu nchini (IDPs) utaratibu kamili na ulio wazi wa usajili wa wakimbizi wa humu nchini na utoaji usaidizi kwao unapswa kuendeshwa sambamba na kuundwa sera ya kutolewa makazi mapya itakayoshughulikia wale wote ambao bado hawana makazi baada ya kutimuliwa makwao wakati wa fujo. Sera hiyo inapaswa kuwa na ratiba inayoonyesha wakati ambapo kutimuliwa watu makwao kutakoma.

Shukrani (Acknowledgements)

ICTJ ingependa kushukuru kwa dhati wenzi waliofaulisha utafiti huu. Wenzi hao ni pamoja na Serikali za Uholanzi (Netherlands), Finland, na Luxembourg na vilevile kundi la asisi na makundi ya waarhiriwa na wawakilishi wao katika Nairobi na kwingineko nchini Kenya ikiwa ni pamoja na Kundi la Waliotimuliwa kutoka Makwao humu Nchini (IDPs Network), Kundi la Haki za Binadamu la Baringo, Kundi la Haki za Binadamu la Eneo la Mlima Kenya, Kundi la Taifa la Waathiriwa, Chama cha Waliopigana Kwenye Vita vya Mau Mau, Kituo cha Utafiti cha Ndula, Kundi la Walioteswa (Torture Victims' Network), Kundi la Wanawake la Maendeleo Mashambani (Women's Rural Development Network), Wanawake katika Matatizo Makali (Women in Crisis), Tume ya Kitaifa ya Kenya ya Haki za Binadamu (KNCHR), Tume ya Kikatoleki ya Haki na Amani (CJPC), Tume ya Haki za Binadamu ya Kenya (KHRC), Shirika la Wanasheria wa Kike (FIDA), Muungano wa Kupambana na Utumiaji Nguvu Dhidi ya Wanawak (COVAW), Asisi ya Kiislamu ya Haki za Binadamu (MUHURI), Kundi la Haki Ijulikane (TBT), na Kundi la mashirika yasiyo ya Kiserikali (CSOs Network)

ictj briefing

“Kuishi Kama Wakenya Wengine”: Utafiti Kuhusu Madai ya Waathiriwa wa Ukiukaji Haki za Binadamu Nchini Kenya

international center for TRANSITIONAL JUSTICE

Kuhusu ICTJ (About ICTJ)

Kituo cha Kimataifa cha Haki ya Kipindi Mpito (ICTJ) inashughulika na kuzuia ukiukaji mkali wa haki kwa kukabiliana na mazoea ya ukiukaji haki dhidi ya umma. ICTJ inalenga suluhisho pana ili kustawisha uwajibikaji na kuunda jamii zenye haki na amani.

ICTJ Nairobi
Lenana Road ACS Plaza
P.O. Box 2193-00202
Nairobi Kenya
Tel: +254-20-3877508
Fax: +254-20-3877663